



## **Tanzania Association of Tour Operators**

CCM District Building, Fire Road  
E+-mail: [tato@cybernet.co.tz](mailto:tato@cybernet.co.tz) <http://www.tatotz.org>

P. O. Box 6162, Arusha, Tanzania

Tel/Fax: 027-2506430  
Tel : 027-2504188  
Mobile : 0784-281170

### **MSIMAMO WA TATO KUHUSU USITISHWAJI WA OPERESHENI TOKOMEZA UJANGILI.**

TATO IMEPOKEA KWA MASIKITIKO MAKUBWA MAJANGA YA WATU KUPOTEZA MAISHA YAO KATIKA OPERESHENI TOKOMEZA UJANGILI.

TUNA IMANI KUWA MAAFA HAYA YA WATU KUPOTEZA MAISHA YAO HAYAKUFANYWA KWA MAKUSUDI NA POLISI, JESHI LETU LA WANANCHI, PAMOJA NA RANGERS AMBAO WALIHUSIKA NA OPERESHENI HII. HAKIKA HAWAKUFANYA HIVI KWA MAKUSUDI YA KUPOTEZA MAISHA YA BINAADAMU, BALI KATIKA VITA VYA AINA YOYOTE ILE MAJANGA HUTOKEA. KWANI "VITA HAVINA MACHO"

KATIKA HOTUBA YA MHESHIMIWA RAIS WA JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA NA AMIRI JESHI MKUU KUHUSU KUSITISHWA KWA OPERESHENI HII, IMETOA NAFASI YA USHINDI KWA MAJANGILI..(TUNAMSHAURI MHE. RAIS PAMOJA NA SERIKALI KUREJEA UAMUZI WA KUSITISHA ZOEZI HILI (TOKOMEZA UJANGILI) NA KULIRUDISHA KWA HARAKA IWEZEKANAVYO KWANI KUTOKOMEA KWA MALI ASILI NI JANGA LA KITAIFA KWA VIZAZI VYA LEO NA VIJAVYO.

TUNATEGEMEA JESHI LETU LITATANGULIZA UTU, HAKI ZA KIBINAADAM NA ULINZI WA RAIA HATA KAMA NI WAHALIFU NA KUWAFIKISHA KWENYE VYOMBO VYA SHERIA. TUNA IMANI KWAMBA ZOEZI HILI (TOKOMEZA UJANGILI..) LINaweza KUFANYIKA SAMBAMBA NA UCHUNGUZI WA VIFO NA WATU KUPOTEZA MAISHA YAO NA WAHUSIKA KUCHUKULIWA HATUA ZA KISHERIA.

TUNAWAPA POLE WALE WOTE WALIOJERUHIWA NA WALIOPOTEZA NDUGU AU JAMAA ZAO KATIKA ZOEZI.

### **HAIWEZEKANI KUWAPA USHINDI MAJANGILI.**

TATO INAPENDA KUIHAKIKISHIA SERIKALI NA WADAU WENGINE USHIRIKIANO WA  
HALI NA MALI PINDI TUTAKAPOHITAJIKA.

WENU MTIIFU

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Wilbard Chambulo', with a stylized flourish extending to the right.

WILBARD CHAMBULO

**MWENYEKITI WA TATO**